# Wafa kwa kufukiwa na kifusi mgodini

**Na Stephano Mango, Songea**

WAKAZI wawili wa eneo la machimbo la Masuguru lililopo katika kijiji cha Amani Makoro wilayani Mbinga, Ruvuma, Thabiti Nyoni (25) na Dominikusi Chusi (25), wamekufa papo hapo baada ya kufukiwa na kifusi cha udongo wakati wakichimba madini.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana Kamanda wa Polisi mkoa wa Ruvuma, Michael Kamuhanda, alisema tukio hilo lilitokea Mei 28 mwaka huu majira ya saa 7:00 mchana.

Alisema siku hiyo ya tukio watu hao walikuwa kwenye eneo walilofikwa na mauti hayo wakati wakitafuta madini aina ya Safaya.

Alisema baadaye watu waliokuwa jirani walikwenda eneo la tukio na kufukua kifusi hicho kwa lengo la kuwaokoa na baadaye kufanikiwa kutoa miili kwa ushirikiano pia wa askari polisi waliofika wakiwa wameambatana na Mganga wa hospitali ya wilaya ya Mbinga.

# Vyanzo vinavyopunguza thamani ya ngozi vyatajwa

**Na Ambrose Wantaigwa, Tarime**

UFUGAJI usiozingatia kanuni za ubora,aina duni za mifugo,elimu duni kwa wafugaji na hali mbaya ya miundombinu ya machinjio vimeelezwa kuchangia kupunguza thamani ya ngozi inayozalishwa hapa nchini.

Mwenyekiti wa Umoja wa wasimamizi wa uzalishaji na usindikaji ngozi nchini(TSHSLP),Kakuru Lugembe, alisema hayo jana wakati wa kikao cha wadau wa sekta ya ngozi kutoka Kanda ya Ziwa kilichoketi mjini hapa kwa lengo la kuwezesha zao hilo kuingia katika ushindani wa soko la ndani na nje.

Alisema ingawa zao la ngozi limeendelea kutoa ajira na kuboresha kipato cha wafugaji,wafanyabiashara na wadau wengine na kuchangia pato la Taifa uzalishaji wake umekabiliwa na changamoto lukuki hivyo kupunguza ubora na thamani yake ndani na nje ya nchi.

Alisema mkakati wa kuendeleza sekta na viwanda vya ngozi nchini ulianza tangu mwaka 2007 lengo kuu likiwa kufufua sekta hiyo ili kuongeza uzalishaji,uboreshaji,ukusanyaji na utengenezaji wa bidhaa itakayohimili ushindani wa kibiashara.

Naye Kaimu mkurugenzi wa Halmashauri ya wilayani hapa Magreth Momburi, alisema baadhi ya wazalishaji wa zao hilo wilayani hapa wamekata tamaa kutokana na kukosa soko la kuaminika hapa nchini na kuamua kusafirisha ngozi kwenda nchi jirani.

# Mashirika ya Ukimwi yapatiwa ruzuku

**Na Neema Kishebuka, Tanga**

MASHIRIKA manne yanayojishughulisha na mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi Vya Ukimwi Jijini hapa yamepatiwa ruzuku ya mkataba wa kufanya kazi na Shirika lisilo la kiserikali la Jiepiego kupitia mradi wake wa Uhai CT

Makabidhiano hayo yaliyofanyika jana mbele ya Katibu Tawala wa mkoa wa Tanga Benedict Ole Kuyang,yalizihusisha taasisi hizo za kijamii ambazo ni Tanga Aids Working Group, TAYODEA, SHDEPHAT na CAN Associates.

Katibu tawala huyo alisema kuwa malengo mazuri ya Shirika la Jiepiego yatawezesha kupunguza maambukizi ya VVU hasa katika maeneo ambayo ni hatarishi zaidi.

"Endapo taasisi zilizobahatika kupatiwa mkataba wa Ruzuku wa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU katika jamii yetu nina imani ya kuwa tutafanikiwa ukizingatia kuwa mradi umelenga maeneo ambayo yapo katika hatari zaidi," alisema Katibu Tawala huyo.

Alizitaka taasisi hizo ambazo zimechaguliwa katika utekelezaji wa mpango huo kuelewa wajibu wa kufanikisha malengo mradi huo ili kuuwezesha mkoa wa Tanga kutekeleza lengo la sita la milenia la kupunguza na kukomesha maambikizi ya ukimwi.

Naye Mkurugenzi wa Jhpiego Hally Mahler, aliliambia gazeti hili kuwa tangu kuanzishwa kwa programu ya Uhai Ct zaidi ya watu 300,000 wa rika na kada mbalimbali wameweza kupima afya zao na kupatiwa ushauri nasaha.

Alisema mradi huo utakaohusisha mikoa ya Tanga, Tabora na Iringa mikoa ambayo ipo katika kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU unafadhiliwa na Shirika la misaada la Marekani (USAID).

# Vibanda vya wafanyabiashara Moshi vyavunjwa

**Na Rodrick Mushi, Moshi**

UONGOZI wa Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro,umevunja vibanda vilivyokuwa vimejengwa na wafanyabiashara wadogo katika eneo la Manyema kwa madai ya kukiuka taratibu ya ujenzi wake.

Vibanda hivyo vilivunjwa usiku wa kuamkia jana baada ya wafanyabiashara hao kudaiwa kukiuka taratibu zilizowekwa na Manispaa hiyo kuwataka kutojenga vibanda hivyo.

Akizungumzia tukio hilo jana Meya wa Manispaa ya Moshi Jafary Maiko, alisema wafanyabiashara hao hawakutakiwa kujenga vibanda kama walivyofanya kwani tayari walishakaa vikao na wafanyabiashara hao na kuwataka kutojenga vibanda hivyo.

Kwa mujibu wa Meya huyo, eneo hilo lingepaswa kutumiwa na wafanyabiashara wadogo waliokuwa wakifanya biashara katikati ya mji(wamachinga) ili kuweza kufanya biashara kwa kupanga bidhaa zao chini.

Ujenzi wa vibanda hivyo vilivyobomolewa na Manispaa havina muda mrefu tangu wafanyabiashara kuhamishiwa katika eneo hilo la Manyema na Manispaa ya Moshi,kwa madai ya wafanyabishara wadogo kuonekana kero katikati ya mji.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO

MASAHIHISHO

## TANGAZO LA KUANZA KUTOA HUDUMA KWA WILAYA ZA ILALA

TUNAPENDA KUWATANGAZIA RASMI KUWA SHIRIKA LA UMEME MKOA WA ILALA LIMEFUNGUA RASMI OFISI ZA WILAYA ZA TABATA, GONGO LA MBOTO NA VIWANDANI KUANZIA TAREHE 2 APRIL 2011. DHUMUNI KUBWA LA KUFUNGUA OFISI HIZI NI KUWA KARIBU ZAIDI NA WATEJA WETU NA HIVYO KUWAFIKIA KWA HARAKA KATIKA KUTOA HUDUMA ZETU. HII NI KATIKA MIKAKATI YETU YA KUBORESHA HUDUMA ZETU KWA WATEJA.

1. Meneja wa Mkoa wa Ilala: Eng. Innocent G. Luoga
Namba ya Simu ni 0768 929296
Namba za Ofisi: 2133332

2. OFISI ZA WILAYA

2.1 WILAYA YA TABATA
Mahali: Tabata Liwiti – Posta jirani na shule ya msingi ya Liwiti
Meneja wa Wilaya: Eng. Felician Makota
Namba ya simu: 0767 303 510
Namba za ofisi : 0684 001 068 na 0715 768 589

Maeneo yatakayohudumiwa: Tabata Kinyerezi, Bonyokwa, Tabata Kisukuru, Segerea, Tabata Bima, Tabata Chang'ombe, Tabata Mawenzi, Tabata Msimbazi na Tabata Matumbi/Dampo

2.2 WILAYA YA VIWANDANI
Mahali: Jengo la TAZARA –Makutano ya barabara ya Nyerere na Mandela
Meneja wa Wilaya : Eng. Madda Mfinanga
Namba ya simu : 0769 832 696
Namba za ofisi: 0684 001 066 na 0715 768 587

Maeneo yatakayohudumiwa: Viwanda vyote vilivyopo barabara ya Nyerere, Uwanja wa Ndege wa JKN, Air Wing, Kiwalani, Kipawa, Vingunguti, Tazara, Vingunguti chogeza, Buguruni Mnyamani, Buguruni Al-Hamza, Buguruni Kimbengele na Karakata

2.3 WILAYA YA GONGO LA MBOTO
Mahali: Banana jirani na kituo cha Hali ya Hewa
Meneja wa Wilaya : Ms. Ludia Kiangi
Namba ya simu : 0767 902 357
Namba za ofisi: 0684 001 071 na 0715 758 584

Maeneo yatakayohudumiwa: Gongo la Mboto yote, Kipunguni, Kitunda, Kivule, Mwanagati, Ukonga Mombasa, Ukonga Magereza, Majumba Sita, Sitakishari, Mong'olandege, Ulongoni na Pugu Mnadani

2.4 WILAYA YA ILALA
Mahali: Jengo la Wizara ya Nishati na Madini (Zamani makao makuu ya TANESCO)
Namba za ofisi : 2 133 330, 0784 768 586 na 0715 768 586

Maeneo yatakayohudumiwa: Upanga yote, City Centre, Kariakoo, Gerezani, Mnazi Mmoja, Muhimbili, Ilala, Buguruni kwa Malapa, Buguruni Kisiwani, Buguruni Sokoni, Buguruni kwa Madenge, Buguruni Moto/Ghana

HUDUMA ZITOLEWAZO NA OFISI HIZI ZA WILAYA NI:
1. Huduma zote za dharura
2. Upimaji na ujenzi wa service line
3. Ukarabati wa miundo mbinu
4. Usomaji na Ukaguzi wa mita na majengo
5. Ubadilishaji wa mita mbovu
6. Ujenzi wa laini kubwa na ndogo

3.0 KITUO CHA HUDUMA KWA NJIA YA SIMU (CALL CENTRE)
Kituo hiki pia kinapokea na kuhudumia wateja wote wa umeme jijini Dar Es Salaam na Kibaha kwa wakati wote wanaohitaji huduma katika Nyanja zifuatazo:-

- Huduma za dharura
- Taarifa za muongozo kuhusu huduma mbalimbai zinazotolewa na Shirika kama vile (kuweka umeme kwenye jengo; ankara za umeme za kila mwezi; njia mbalimbai za kununua umeme wa LUKU kama vile ZAP, M-PESA, MAXMALIPO, NMB mobile)
- Taarifa za upatikanaji wa huduma ya umeme hususani ratiba ya mgao wa umeme.

Namba za simu 022 2194 400

Imetolewa na: OFISI YA MAWASILIANO,
TANESCO - MAKAO MAKUU.

# Uwezo wazindua tathmini ya elimu kwa wilaya 133

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa Uwezo ambao upo chini ya Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) jana umezindua tathimini ya kupima uwezo wa watoto wa kusoma, kufanya hesabu rahisi kwa wilaya 133 nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es salaam, Meneja Utafiti wa Uwezo Tanzania, Dk. Grace Soko, alisema tathimini hiyo itakayoanza Mei mwaka huu ni ya pili baada ya ile ya Mei mwaka jana ambayo ilihusisha wilaya 38.

Alisema katika tathimini ya mwaka jana ambayo matokeo yake yalizinduliwa Septemba, yalibaini kuwa mmoja kati ya wahitimu watano wa elimu ya msingi nhawezi kusoma kuswahili cha ngazi ya pili, nusu ya wahitimu wa elimu hiyo hawawezi kusoma Kiingereza na watatu kati ya 10 hawawezi hisabati za ngazi ya dara sa la pili

Alibainisha kuwa tathimini hiyo iliwalenga watoto kati ya miaka 5-16 na ilifikia kaya 22,800 katika vijiji 1,140 ambapo zaidi ya watoto 42,000 walijaribiwa kwa kupewa mazoezi ya hisabati, Kiingereza na Kiswahili

Aliongeza kuwa mwaka huu Uwezo inatarajia kufikia kata 80,000 ambapo waratibu waliopatiwa mafunzo wataanza kuorodhesha kaya hizo na baadae watafanya tathimini hiyo kwa kushirikiana na watu watakaojitolea.

Alisema ili kufanikisha zoezi hilo Uwezo imeamua kufanya mafunzo ya kitaifa kwa waratibu wa wilaya hizo 133 ambao baadaye watawafunza wakusanya taarifa waliojitolea na kusimamia zoezi hilo.

Naye Mwenyekiti wa TEN/MET, Ginason Jandwa, alisema kuwa baada ya utafiti wa mwaka jana kuna baadhi ya wizara na idara za serikali zilikuwa zikisuasua kuwapa ushirikiano lakini baada ya muda walizungumza na wanashirikiana vizuri.

Uwezo Tanzania ni mradi wa miaka minne unaolenga kukuza ustadi wa kusoma, Kiingeraza, Kiswahili na ujuzi wa hesabu kwa watoto wenye umri wa miaka 5-16.



MAZUNGUMZO

**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi wa Ireland nchini, Lorcan Fullam, wakati balozi huyo alipomtembelea Rais Shein, Ikulu mjini Zanzibar, jana. (Picha na Ramadhan Othman wa Ikulu).**

# Wajawazito 48 wafa kwa kucheleweshwa vituo vya afya

**Na Ahmed Makongo, Kahama**

WANAWAKE wajawazito 48 wamepoteza maisha wilayani Kahama, Shinyanga mwaka jana kutokana na matatizo ya kujifungua, huku baadhi yao sababu kubwa ikiwa ni kuchelewa kufika kwenye vituo vya afya.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Khama, Dk. Leonard Subi, alibainisha hayo alipokuwa akijibu maswali ya wananchi kwenye mkutano wa hadhara, uliokuwa unahutubiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Ezekiel Maige, katika Kijiji cha Bugalama, wilayani Kahama.

Dk. Subi alitoa takwimu hizo, baada ya Naomi Stephen, kusema kuwa wanawake wajawazito katika kijiji hicho wamekuwa wakitaabika wakati wa kujifungua kutokana na kutokuwepo kwa huduma nzuri za afya katika zahanati ya kijiji hicho.

Naomi pamoja na wananchi mbalimbali walimuomba Waziri Maige, ambaye pia ni Mbunge wa Msalala, kufanya kila liwezekanalo ili zahanati hiyo iweze kuboreshwa na kutoa huduma zinazostahili ili kupunguza adha kwa wananchi.

Akijibu kero hiyo, Dk. Subi alisema idara ya afya wilayani humo pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili, imekuwa ikijitahidi kuboresha zahanati, lakini tatizo lililopo ni baadhi ya wajawazito kutokuhudhuria kiliniki.

Kwa upande wake Waziri Maige, alisema serikali inatambua changamoto mbalimbali zinazoikabili idara ya afya, na kusema kuwa ahadi zote ambazo serikali ilizitoa zitatekelezwa ndani ya kipindi cha miaka mitano.

# TTB yashinda tuzo za ubora

**Na Chalila Kibuda**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) imeshinda tuzo mbili za ubora katika maonyesho ya kimataifa ya utalii yaliyoshirikisha washiriki zaidi ya 400 duniani, yanayojulikana kama Outbound Travel Market (OTM) yaliyofanyika nchini India.

TTB imeshinda tuzo hizo kwa nyakati tofauti katika maonyesho hayo yaliyofanyika Februari mwaka huu nchini India.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Masoko wa TTB, Geofrey Meena, alisema tuzo hizo zinaonyesha mafanikio wanayopata TTB katika mikakati yao ya kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini katika nchi mbalimbali duniani ambapo banda la bodi hiyo limekuwa likiwavutia watu wengi.

Alifafanua kuwa vivutio vya utalii vilivyotumika kupamba banda la bodi hiyo pamoja na bidhaa za kitamaduni vilichangia kwa kiasi kikubwa kuipa ushindi Tanzania, ambapo vivutio vya wanyamapori na milima viliwavuta wengi.

"Tumepata tuzo mbili katika maonyesho ya kimataifa yaliyofanyika hivi karibuni ambapo kwetu ni jambo la kujivunia kama bodi, lakini pia ni sifa kubwa kwa nchi ikizingatiwa kuwa tumekuwa na jitihada za makusudi kuutangaza utalii wetu duniani kote," alisema Meena.

Wakati huohuo TTB itakuwa mwenyeji wa watalii 1,000 kutoka nchini India wanaotarajia kuwasili nchini Julai mwaka huu, watalii hao watakapokuwa nchini kwa siku tano watatembelea visiwa vya Zanzibar, mbuga za wanyama za Serengeti na Ngorongoro.

# Polisi wasaka kilo 300 za bangi

**Na Berensi Alikadi, Bunda**

JESHI la Polisi wilayani Bunda, Mara linamshikilia Werema Chacha (36), mkazi wa Kijiji cha Kiwamamba baada ya kukamatwa na kilo 300 za bangi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Boaz Robert, alisema jana kuwa Chacha alikamatwa juzi majira ya saa 4 katika eneo la Mto Rubana wilayani hapa.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, kukamatwa kwa mtu huyo kulitokana na taarifa kutoka kwa raia wema ambao waliwataarifu polisi kuhusu kuwepo kwa dawa hizo.

Alisema baada ya polisi kupewa taarifa hizo waliweka mtego na kufanikiwa kumkamata mtu huyo akiwa nyumbani kwa Adango Tondwe.

Bangi hiyo ilikuwa imefungwa kwenye mifuko ya sandarusi na kuwekewa dagaa kwa ajili ya kuficha harufu yake.

Alifafanua kuwa baada ya askari hao kufika nyumbani hapo wakiongozwa na Mkuu wa kituo hicho, ASP Mayunga, mwenye nyumba hiyo alifanikiwa kukimbia ambapo polisi hao walimkamata mtuhumiwa huyo ambaye alikuwa katika harakati za kuisafilisha bangi hiyo.

Mtuhumiwa huyo anatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya kukamilika kwa upelelezi.

# Mbunge kuwasilisha hoja kufunga mgodi

"Nimelazimika kuwasilisha hoja hiyo kutokana na hasara nyingi wanazopata wakazi wa maeneo hayo zaidi ya faida ikiwa ni pamoja na madhara ya kiafya yanayotokana na uchafuzi wa mazingira kwa sababu mgodi huo umeshindwa kuwalipa fidia ili waishi mbali na shughuli za uzalishaji.

**Na Ambrose Wantaigwa, Tarime**

MBUNGE wa Viti Maalumu mkoani Mara, Esther Matiku (Chadema) anatarajia kuwasilisha hoja binafsi katika vikao vijavyo vya Bunge kuomba kufungwa mgodi wa dhahabu wa African Barrick Gold wilayani hapa kutokana na kushindwa kunufaisha wakazi wanaozunguka eneo hilo pamoja na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Akizungumza na Tanzania Daima kwa njia ya simu jana, alisema licha ya mgodi huo kuendesha uchimbaji wa dhahabu katika eneo hilo, wananchi wa maeneo hayo wamezidi kubaki katika lindi la umaskini.

Alisema ingawa baada ya kubinafsishwa mgodi huo uliweka mikataba midogo midogo kwa pamoja na vijiji ikiwa pamoja na kuchangia katika elimu, maji na miundombinu, lakini bado utekelezaji wake umebaki kuwa sifuri kutokana na wawekezaji hao kubadili majina mara kwa mara na kuondoka huku wananchi wakibaki kama yatima.

"Nimelazimika kuwasilisha hoja hiyo kutokana na hasara nyingi wanazopata wakazi wa maeneo hayo zaidi ya faida ikiwa ni pamoja na madhara ya kiafya yanayotokana na uchafuzi wa mazingira kwa sababu mgodi huo umeshindwa kuwalipa fidia ili waishi mbali na shughuli za uzalishaji.

"Kuna nyumba za makazi ya watu zimepata nyufa kutokana na milipuko ya baruti na kama haitoshi wakazi wa eneo hilo wanapoonekana karibu na mgodi wanaitwa wavamizi," alisema.

Katika hatua nyingine, mbunge huyo ameutaka mgodi huo kutengua uamuzi wake wa kusimamisha malipo ya asilimia 100 uliotumika kugharimia masomo ya wanafunzi kutoka familia maskini katika vijiji vinavyozunguka mgodi huo kwa sababu za kibinadamu, kwa kuwa unaathiri utoaji wa elimu kwa wahusika.

Hivi karibuni mgodi huo kwa maelekezo ya Mkuu wa Wilaya ya Tarime, John Henjewele, ulisitisha mgawo wa asilimia 100 uliokuwa ukitoa kwa vijiji vyote vinavyozunguka mgodi huo kwa madai kwamba kulikuwa na majina hewa zaidi 2,000 yaliyoingizwa kwa msaada wa baadhi ya viongozi wa vijijij wasio waaminifu.